Liberté • Égalité • Fraternité
RÉPUBLIQUE FRANÇAISE

MINISTÈRE DES AFFAIRES ÉTRANGÈRES ET EUROPÉENNES

DIRECTION GENERALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des concours et examens professionnels
RH4B

CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCES A L'EMPLOI DE SECRETAIRE DES AFFAIRES ETRANGERES (CADRE D'ORIENT) AU TITRE DE L'ANNEE 2012

EPREUVES ECRITES D'ADMISSIBILITE

8 septembre – 14 septembre 2011

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures.
Coefficient : 2.
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.
Barème de notation des 3 épreuves : QCM 4 points, fiche 10 points, note 6 points.

– QUESTIONNAIRE A CHOIX MULTIPLES –

*Réponse à un questionnaire à choix multiples portant sur la grammaire, les structures et les usages de la langue swahilie. – **Durée : 30 minutes.***

Ce dossier comporte 3 pages (page de garde non comprise).

*
* *

SUJET :

Compléter la grille de réponse distribuée séparément, une seule réponse par question.

11	Jenerali Ahmar anapendekezwa kushika hatamu ya uongozi ..... watamuondoa Rais Saleh.							
	a	iwapo	**b**	hata	**c**	mpaka		
12	(...) baada ya kikao cha Baraza la usalama la Umoja wa Mataifa ..... rasmi kukataa hoja hiyo ya Kenya.							
	a	kisichokuwa	**b**	hakiwa	**c**	hakilichokuwa		
13	Taarifa zinaonyesha kuwa, sio tu kwamba kakao lililo kwenye mikono ya wasafirishaji linapotea, lakini pia zao hilo linauzwa katika masoko ..... rasmi.							
	a	yasiyokuwapo	**b**	ambayo si	**c**	yasiyo		
14	Hana la kufanya kutokana na athari za mgogoro wa kisiasa ambao umeikumba nchi hiyo ..... kutajwa kama llulu ya Magaribi mwa Afrika.							
	a	iliyokwisha	**b**	iliyowahi	**c**	iliyotaka		
15	Amesema hiyo ni ishara ya kuanza ..... kibiashara.							
	a	kufilisikia	**b**	kufilisiwa	**c**	kufilisika		
16	Katikati ya Februari mwaka huu, zaidi ya tani 400 000 za kakao .....katika bandari za Abidjan na San Pedro.							
	a	zilizuiwa	**b**	zilizuikana	**c**	zilizuilika		
17	Inakadiriwa zaidi ya tani 170 000 ..... kutoka Cote d'Ivoire kwa njia haramu.							
	a	zimehamishiwa	**b**	zimehamishwa	**c**	zimehamasishwa		
18	Wiki chache zilizopita wafanyabiashara ..... zao hilo kwa bei ya kutupa.							
	a	walijinunulia	**b**	walijinunulisha	**c**	walijinunua		
19	Ocampo aidha .....mbali hofu ya kukamatwa kwa washikiwa hao sita.							
	a	aliondoka	**b**	aliondoa	**c**	aliondolea		
20	Lakini ..... ni swala la muda tu.							
	a	inapoonekana	**b**	inavyoonekana	**c**	inayoonekana		

2ème série (10 questions)

Complétez le texte à l'aide des termes qui vous sont donnés

Par exemple : Na njia ya pekee iliyopo sasa ni kukata .....**0**..... mbele ya mahakama hiyo.

0	**a**	rufaa	**b**	kifaa	**c**	kichaa

.....**1**..... mataifa ya Ulaya yakizizuia akaunti za fedha za kiongozi wa Libya, Muammar Gaddafi, kiongozi huyo ana hazina nyingine ya mamilioni kwenye nchi .....**2**..... za Afrika.

Kwa miongo kadhaa sasa, kiongozi huyo amekuwa akiwekeza katika miradi mikubwa mikubwa ya ujenzi wa .....**3**....., huduma na usafiri katika bara hilo. Kampuni ya taifa ya mafuta ya Libya .....**4**....., ina mtandao wa matangi 2000 ya mafuta katika nchi 20 za Afrika.

Ni rahisi kwenye nchi za Afrika kukuta barabara inayoitwa mtaa wa Gaddafi, au msikiti wa Gaddafi, au jengo la Gaddafi, maana nchi nyingi za bara hilo zinamtukuza kiongozi huyo.

Na hili, hapana shaka, linaonyesha namna ambavyo Gaddafi amekuwa na ushawishi katika sehemu kadhaa za bara hilo.

Kwenye Benki ya Maendeleo ya Afrika peke yake ina .....**5**..... wa euro milioni 260, jambo ambalo mwakilishi wa benki hiyo ya kanda ya Afrika ya Kaskazini, Emanuele Santi, anaona halitabadilika. « Libya ni mshirika muhimu kwenye benki yetu. Sifikirii kuwa Gaddafi atazitoa fedha zake, ...**6**..... daima amekuwa akionyesha mshikamano na bara la Afrika na kwa hivyo hawezi kubadilika. Na sisi pia hatukusudii kuzizuia fedha zake. »

.....**7**....., thamani ya .....**8**..... uchumi mbalimbali vya Libya kwenye nchi mbalimbali za Afrika inafikia euro bilioni sita. Miradi na makampuni kadhaa makubwa yanafaidika na mkopo wa kifedha kutoka Libya. Mfano ni kampuni ya simu ya Uganda Telecom, ambayo mbili ya tatu ya .....**9**..... zake inamilikiwa na mamlaka ya Uwekezaji ya Libya, ambayo thamani yake ni karibu euro milioni 10. Na kama hilo halitoshi, katika miaka ya hivi karibuni, Gaddafi (...) aliahidi mabilioni zaidi ya euro .....**10**..... kwenye uchumi wa bara la Afrika. (DW-World.de25/03/2011)

1	**a**	kwa hivyo	**b**	huku	**c**	kwa sababu
2	**a**	kadhaa	**b**	sawa	**c**	mpya
3	**a**	harakati	**b**	migodi	**c**	miundombinu
4	**a**	peke yake	**b**	upweke	**c**	ya kipekee
5	**a**	utajiri	**b**	mtaji	**c**	mali
6	**a**	pamoja na	**b**	hata hivyo	**c**	maana
7	**a**	mwishowe	**b**	kwa ujumla	**c**	kwa kuwa
8	**a**	mtego	**b**	vitega	**c**	utingo
9	**a**	hisia	**b**	hisa	**c**	hesi
10	**a**	kuwekwa	**b**	kutiwa	**c**	kuwekezwa

Liberté • Égalité • Fraternité
RÉPUBLIQUE FRANÇAISE

MINISTÈRE DES AFFAIRES ÉTRANGÈRES ET EUROPÉENNES

DIRECTION GENERALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des concours et examens professionnels
RH4B

CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCES A L'EMPLOI DE SECRETAIRE DES AFFAIRES ETRANGERES (CADRE D'ORIENT) AU TITRE DE L'ANNEE 2012

EPREUVES ECRITES D'ADMISSIBILITE

8 septembre – 14 septembre 2011

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures.
Coefficient : 2.
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.
Barème de notation des 3 épreuves : QCM 4 points, fiche 10 points, note 6 points.

– FICHE DE SYNTHESE EN FRANÇAIS –

*Rédaction en **français** d'une fiche de synthèse (350 mots avec une tolérance de plus ou moins 10%) à partir de documents en swahili. – **Durée (note et fiche de synthèse) : 2 heures 30 minutes.***

Ce dossier comporte 7 pages (page de garde non comprise).

*
* *

SUJET : Vous rédigerez une fiche en français sur la mort de Fazul Abdullah Mohammed.

13.06.2011

Pigo kubwa kwa al-Qaeda Afrika Mashariki

Kiongozi wa tawi la al-Qaeda katika Afrika Mashariki aliuawa tangu katikati ya wiki iliyopita, lakini ni siku ya Jumamosi ndio alipotambuliwa kwa hakika kuwa huyo ni Fazul Abdullah Mohammed.

Kwanza aliuawa Osama bin-Laden na sasa ni kiongozi wa al-Qaeda katika Mashariki ya Kati. Marekani imesherehekea kifo cha Fazul Abdullah Mohammed kama pigo kubwa dhidi ya mtandao wa kigaidi. Kwa miaka kadhaa, kiongozi huyo wa ugaidi aliweza kujificha na mara kwa mara alikwepa kukamatwa akitumia majina mavazi tofauti. Safari hii alipigwa risasi na kuuawa, baada ya kusimamishwa kwa bahati tu, kwenye kituo cha ukaguzi barabarani, nchini Somalia. Afisa wa serikali ya Marekani amesema, sasa kundi la al-Qaeda limepoteza kiongozi mwenye ujuzi mkubwa wa kupanga operesheni za mtandao huo.

Ukweli ni kwamba kundi hilo la kigaidi, limedhoofika kutokana na kifo cha Fazul Abdullah Mohammed aliekuwa na umri kama miaka 40. Yeye alikuwa mwerewu, mtaalamu wa compyuta, alizungumza lugha tano kwa ufasaha na yeye ndiye aliepanga shambulio la kwanza kabisa la al-Qaeda. Hata kabla ya mashambulizi ya Septemba 11 mwaka 2001, kundi hilo la kigaidi mnamo mwezi wa Agosti mwaka 1998, lilishambulia kwa wakati mmoja, balozi za Marekani nchini Tanzania na Kenya.

Mashambulio hayo yalisababisha vifo vya takriban watu 240. Kuanzia hapo, Fazul Abdullah Mohammed alikuwa katika orodha ya watu wanaosakwa zaidi.

Kufuatia kifo cha Osama bin-Laden, ilichukuliwa kuwa yeye ndio atakaerithi nafasi yake. Inasemekana kuwa wote wawili walikuwa na heba. Wale waliokuwa karibu nao, wamewaeleza kama watu waliokuwa wema, waliotulia na waliokuwa na vipaji vya kuvutia watu.

Na kwa mtandao wa al-Qaeda, Fazul Abdullah Mohammed alikuwa muhimu sana kwani aliweza kuwavutia wafuasi wapya. Yeye alitayarisha kambi za kutoa mafunzo kwa washambuliaji vijana nchini Somalia na aliweza kuwasadikisha kuwa ni sahihi kujitoa mhanga kwa Mwenyezi Mungu. Sasa, tawi la al-Qaeda katika Mashariki ya Kati limeachwa na pengo.

Lakini mtandao wa al-Qaeda hauna shida ya kupata wafuasi wapya, kwani nchini Somalia kuna maelfu ya wanaume vijana, wasiojua chochote isipokuwa vita na wao wapo tayari kujitoa mhanga.

Mwandishi: Diekhans,Antje,ZPR

Mhariri:Miraji Othman

| www.dw-world.de | © Deutsche Welle.

12.06.2011

Fazul Mohammed nguzo ya Al-Qaida iliyoanguka

Wachambuzi wanasema kifo cha mwanamgambo na kiongozi wa al Qaeda katika eneo la Afrika Mashariki Fazul Mohammed kilichotokea nchini Somalia kinaelezwa kuwa ni pigo kubwa katika utekelezaji wa operesheni za mtandao huo.

Kuuawa kwa mwanamgambo wa ngazi za juu wa kundi la kigaidi la al-Qaeda Fazul Mohammed unaliingiza kundi hilo katika majonzi makubwa ikiwa ni mwezi mmoja kufuatia kifo cha Osama bin Laden. Lakini dhima yake ya hivi karibuni kama mkufunzi wa wanamgambo wapya huenda imeacha kitisho kikubwa.

Polisi nchini Somalia jana ilitangaza kwamba Fazul Mohamed, aliekuwa akisakwa muda mrefu na aliekuwa mtaalamu wa kupanga mashambulizi, kujificha, kukwepa kukamatwa na hodari wa lugha aliuawa katika mji mkuu wa Somalia Mogadishu.

Kufuatia tangazo hilo, Marekani ilisema Fazul Mohammed anaejulikana pia kama Harun, ni mshukiwa mkuu kuhusiana na mashambulizi ya 1998 katika balozi za Marekani katika majiji ya Dar es salaam na Nairobi, ambapo watu 240 walipoteza maisha yao.

Inaaminiwa kuwa mzaliwa huyo wa Komoro alipanga shambulio la mwaka 2002 dhidi ya hoteli inayomilikiwa na Israel nchini Kenya na kusababisha vifo vya watu 15.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni, baadhi ya wasomi na wataalamu wa masuala ya usalama waliamini kwamba Fazul Mohamed alikuwa akitumia muda mwingi kutoa mafunzo kwa wanamgambo sawa na kuaanda mipango ya kushambulia nchi za magharibi.Alikuwa akitoa mafunzo kwa vijana wa Kisomali na Waislamu wengine waliokwenda Somalia kupata ujuzi wa kijeshi.

Profesa Nelly Lahoud wa kituo cha kukabiliana na ugaidi katika chuo cha kijeshi cha West Point nchini Marekani anasema, Fazul Mohammed alikuwa mtu muhimu katika kupanga operesheni za mtandao wa al-Qaeda. Amesema kifo chake ni hasara kubwa kwa mtandao huo ingawa jukumu lake la hivi karibuni, kama mkufunzi bila shaka limenufaisha kundi.

Profesa Lahoud aliechunguza kitabu kilichoitwa "Vita dhidi ya Uislamu: Hadithi ya Fazul Harun" ambacho huelezea maisha ya Fazul Mohammed, amesema kuwa mwanamgambo huyo ametoa mchango mkubwa kwa mtanadao wa al Qaeda. Kwa maoni yake, Fazul Mohamed aliihisi kuwa aliwajibika kuwapa wenzake ujuzi aliokuwa nao.

Serikali ya Somalia imesema mamia ya wapiganaji wa kigeni walijiunga na mtandao huo wa kigaidi, wakitokea nchi mbalimbali kama Afghanstan, Pakistan, nchi za Ghuba na za Magharibi zikiwemo Marekani na Uingereza.

Baadhi yao wamekuwa viongozi wa makundi ya wanamgambo kama vile al Shabaab.

Maafisa wa usalama katika nchi za Magharibi pia walikuwa wakishuku kuwa Fazul Mohammed alikuwa akiratibu harakati zao pamoja na wanamgambo wa tawi la al Qaeda nchini Yemen. Hilo ni tawi lililohusika na mashambulizi makali yaliyofanywa na mtandao huo katika nchi za magharibi, miaka ya hivi karibuni.

Maafisi wa usalama waliomchunguza Fazul Mohammed wanasema alikuwa mtu makinifu na mjanja na aliezungumza lugha za Kiarabu, Kikomoro, Kiswahili na Kiingereza.

Muaustralia Leah Farrell alie mtaalamu wa masuala ya al-Qaeda, amesema ni kifo cha Fazul Mohamed kitaathiri uwezo wa al-Qaeda kuwepo katika kanda hiyo pamoja na operesheni zake katika nchi za kigeni.

Baadhi wa wataalamu wa masuala ya usalama, wanashuku kwamba mafunzo yaliyotelowa na Fazul Mohammed yamesaidia kupanga shambulio lililofanywa na kundi la al-Shabab mjini Kampala, Uganda mwaka 2010. Shambulio hilo limesababisha vifo vya watu 79 waliokuwa wakitazama fainali ya kombe la dunia.

Hilo lilikuwa shambulio la kwanza kabisa kufanywa na al Shebab katika nchi ya kigeni, kulipiza kisasi baada ya Uganda kuchangia wanajeshi katika kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Afrika nchini Somalia-AMISOM. Katika shambulio lingine, wanamgambo wa al-Shabaab walishambilua kambi kuu ya jeshi la Umoja wa Afrika Septemba 2009, mjini Mogadishu. Wanajeshi 17 waliuawa katika mashambulio mawili ya mabomu yaliyotegwa katika gari.

Kufuatia kifo cha Fazul Mohammed, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Hillary Clinton alikaribisha habari hiyo akiwa ziarani nchini Tanzania. Aliwaambia waandishi wa habari kuwa kifo cha Fazul Abdullah Mohamed ni " pigo kubwa" kwa al-Qaeda na washirika wake katika kanda hiyo.

Mwandishi: Sudi Mnette / RTR

Prema Martin

| www.dw-world.de | © Deutsche Welle.

11 Juni, 2011 - Imetolewa 15:57 GMT

Marekani yathibitisha kifo cha Fazul

Waziri wa mashauri ya nje wa Marekani Bi Hillary Clinton, amesema kifo cha Fazul Abdullah Mohammed, aliyeshukiwa kuwa mkuu wa Al Qaeda Afrika Mashariki, "ni pigo kubwa" kwa kundi hilo na washirika wake.

Jumamosi serikali ya Marekani imethibitisha kifo cha Fazul Abdullah Mohammed, katika tukio la kufyatuliana risasi na vikosi vya Somalia mjini Mogadishu.

"Kifo cha Harun Fazul ni pigo kubwa kwa Al Qaeda, washirika wake wa siasa kali, na shughuli zake Afrika Mashariki," Clinton aliwaeleza waandishi wa habari akiwa mjini Dar es Salaam, Tanzania.

"Ni mwisho unaostahili kwa gaidi aliyewaletea wengi kifo na huzuni watu wasiokuwa na hatia Nairobi, Dar es Salaam na kwingineko; Watanzania, Wakenya, Wasomali na wafanyakazi wetu wa ubalozi".

Awali afisa mmoja wa cheo cha juu katika serikali ya Marekani alithibitisha kifo cha kiongozi huyo wa Al Qaeda Afrika Mashariki, na kuipongeza serikali ya muda nchini Somalia.

Kiongozi huyo wa Al Qaeda katika kanda ya Afrika ya Mashariki Fazul Abdullah Mohammed, alishukiwa kuhusika na shambulio dhidi ya balozi za Marekani katika Kenya na Tanzania mnamo mwaka 1998.

Alishukiwa kuhusika na milipuko ya balozi za Marekani katika miji ya Nairobi na Dar es Salaam

Fazul Abdullah amekuwa mtu anayetafutwa sana barani Afrika baada ya zaidi ya watu 220 kuuawa na zaidi ya 5000 kujeruhiwa katika mashambulio ya mwaka 1998.

FBI iliahidi dola milioni 5 kwa kichwa chake

'Pasi ya kigeni'

Maafisa wa usalama wa nchini Somalia wameyaambia mashirika ya habari ya AFP na Reuters kuwa Fazul Abdullah na mwenzake waliuawa kwa kupigwa risasi na wanajeshi wa serikali ya mpito ya Somalia katika kizuizi cha barabarani siku ya Jumatano.

"Vikosi vyetu viliwafyatulia risasi wawili hao waliokataa kusimama katika kizuizi cha barabarani. Walijaribu kujitetea walipozingirwa na askari wetu," kamanda wa majeshi ya serikali ya mpito ya Somalia Abdikarim Yusuf ameliambia shirika la habari la AFP.

"Tulichukua vitambulisho vyao vikiwemo pasi ya kigeni pamoja na dawa, simu za mkononi na komputa za laptop," akaongeza.

Duru za maafisa wa Somalia zimeifahamisha AFP kwamba Fazul alikuwa amebeba kiasi cha dola elfu 40,000 taslimu na pasi ya kusafiria ya Afrika Kusini ikiwa na jina "Daniel Robinson".

Pasi hiyo iliotolewa Aprili 13, 2009, ikionyesha kwamba aliondoka Afrika Kusini Machi 19, 2011 kuelekea Tanzania, ambako alipewa kibali cha kuingia.

Afisa mwaandamizi wa usalama nchini Somalia Hatima Aden, amethibitisha kuwa Fazul aliuawa katika kizuizi cha barabarani, wiki hii na kwamba alikuwa na pasi ya Afrika Kusini.

"Baada uchunguzi tulithibitisha kuwa ni yeye na tukamzika," aliliambia shirika la habari la Reuters.

Mkuu wa polisi wa Kenya , Matthew Iteere, amewaambia waandishi habari mnamo siku ya Jumamosi kwamba anashauriana na maafisa wa Somalia kupata ripoti kamili.

"Tumeambiwa kulikuwa na magaidi wawili waliouawa nchini Somalia mnamo siku ya Jumaatano. Walitajwa kuwa ni Fazul Mohammed na Ali Dere. Hayo ndio tulioelezwa na wenzetu," aliviambia vyombo vya habari nchini Kenya.

Hata hivyo msemaji wa vikosi vya kulinda amani vya Muungano wa Afrika nchini Somalia amesema picha za matti hazielekei kuwa zinafanana na Fazul Abdullah Mohammed.

Kundi la wapiganaji wa Kiislamu la Al Shabab limesema taarifa za kuuawa kwake si kweli.

Fazul Abdullah alizaliwa katika visiwa vya Comoro katika miaka ya 1970, na inaaminiwa alijiunga na kundi la al-Qaeda nchini Afghanistan katika miaka ya 1990.

Baada ya mashambulio ya balozi za Marekani katika miji ya Nairobi na Dar es Salaam, Tanzania, mwaka 1998, ambapo watu 224 waliuwawa; Marekani iliimshtumu kwa kuhusika na kutoa tuzo za dolla milioni 5 kwa mtu yeyote atakayetoa habari zitakazosababisha kukamatwa kwake.

Mnamo mwaka 2002, Abdullah pia alishtumiwa kwa kuhusika na mashambulio dhidi ya hoteli ya Kikambala mjini Mombasa, Kenya na jaribio la kuidungua ndege ya shirika la Israel.

Mwaka 2007, alinusurika shambulio la ndege za kivita za Marekani katika kijiji cha Haya, kusini mwa Somalia, karibu na mji wa Ras Kamboni.

FAZUL ABDULLAH MOHAMMED: Nguzo muhimu ya Al-Qaida iliyoanguka

Posted By admin On June 15, 2011 @ 11:20 am In Habari za kimataifa,Mtanzania | No Comments

- Ni mkali wa lugha tano ikiwamo Kiswahili
- 'Alishuhudia' MV Bukoba ikizama

Joseph Hiza na Mashirika ya Habari

KIONGOZI wa Mtandao wa Kigaidi wa Al-Qaeda kwa ukanda wa Afrika Mashariki, Fazul Abdullah Mohammed ameuawa na Jeshi la Serikali ya Mpito la Somalia usiku wa kuamkia Jumatano ya wiki iliyopita.

Kifo hicho ni pigo kubwa katika utekelezaji wa operesheni za mtandao huo eneo hili na kwingineko kwa ujumla wake.

Kuuawa kwake kunaliingiza kundi hilo katika majonzi makubwa ikiwa ni mwezi mmoja tu tangu kuuawa kwa kiongozi mkuu wa mtandao huo duniani, Osama

Lakini dhima na kazi yake aliyoijenga katika miaka mchache iliyopita kama mkufunzi wa wanamgambo wapya huenda ikawa imeacha tishio kubwa kwa usalama wa eneo hili sasa na siku za usoni.

Kwa mujibu wa polisi wa Somalia, Fazul Mohamed, aliyekuwa akisakwa kwa muda mrefu na aliyekuwa mtaalamu wa kupanga mashambulizi, kujificha, kukwepa kukamatwa na mahiri katika kuzungumza lugha mbalimbali aliuawa wakati wa mrushiano wa risasi katika mji mkuu wa Somalia, Mogadishu.

Maafisa wa Somalia juzi walisema Fazul ambaye Marekani ilimtangazia 'bingo' yenye thamani ya dola za Marekani milioni tano kwa yeyote atakayetoa taarifa zitakazosaidia kukamatwa kwake, aliuawa akiwa na mtuhumiwa mwingine wa ugaidi baada ya kufyatuliana risasi na polisi kwenye kizuizi cha barabara karibu na Mogadishu.

Kufuatia kifo cha Fazul Mohammed, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Hillary Clinton, alikaribisha habari hiyo akiwa ziarani nchini Tanzania.

Aliwaambia waandishi wa habari kuwa kifo cha Fazul Abdullah Mohamed ni 'pigo kubwa' kwa al-Qaeda na washirika wake katika kanda hiyo.

Tangazo la vifo hivyo lilicheleweshwa kusubiri vipimo vya DNA kuthibitisha utambulisho wake pamoja na picha.

Awali askari waliomuua hawakuwa wamemtambua.

"Tulimzika," anasema Jenerali Abdikarim Yusuf Dhagabadan, Naibu Mkuu wa Jeshi la Somalia.

"Lakini mara tulipokagua nyaraka zake, na kubaini kitu tuliufukua mwili wake na kuchukua picha na vipimo vya DNA.

Tukabaini ni mtu aliyekuwa akisakwa na mamlaka za Marekani."

Jenerali huyo anakieleza kifo hicho kama kile cha Osama bin Laden.

"Ni ushindi kwa dunia. Ni ushindi kwa Jeshi la Somalia," anaongeza.

Mkuu huyo wa Al-Qaeda Afrika Mashariki alikuwa katika gari aina ya Pickup lililokuwa limejaa dawa, kompyuta za laptop na simu za mkononi akijaribu kuelekea katika eneo linalodhibitiwa na waasi.

Inaonekana Fazul na mwenzake ambaye baadaye alikuja fahamika kuwa Ali Dele walifanya kosa lililowagharimu katika kizuizi cha barabara na walikataa kusimama, kwa mujibu wa maofisa, hali iliyosababisha kufyatuliana risasi kulikogharimu maisha yao.

"Vikosi vyetu viliwafyatulia risasi wawili hao waliokataa kusimama katika kizuizi cha barabara. Walijaribu kujitetea walipozingirwa na askari wetu," Abdikarim analiambia Shirika la Habari la Ufaransa (AFP).

"Tulichukua vitambulisho vyao ikiwamo hati za kusafiria za kigeni pamoja na dawa, simu za mkononi na kompyuta za laptop," anaongeza.

Maofisa wa Somalia wamesema Fazul alikuwa amebeba kiasi cha dola za Marekani 40,000 taslimu na hati ya kusafiria ya Afrika Kusini ikiwa na jina 'Daniel Robinson.'

Pasi hiyo iliyotolewa Aprili 13, mwaka juzi, ikionyesha aliondoka Afrika Kusini Machi 19, 2011 kuelekea Tanzania, ambako alipewa kibali cha kuingia.

Fazul Mohammed anayejulikana kwa jina lingine la Harun, ni mshukiwa mkuu wa mashambulizi ya mwaka 1998 katika balozi za Marekani mjini Dar es Salaam-Tanzania na Nairobi-Kenya, yaliyoua watu 240.

Inaaminika mzaliwa huyo wa Comoro pia alipanga shambulio la mwaka 2002 dhidi ya hoteli inayomilikiwa na Wayahudi mjini Mombasa, Kenya na kusababisha vifo vya watu 15.

Lakini katika miaka michache iliyopita, baadhi ya wasomi na wataalamu wa masuala ya usalama waliamini Fazul Mohamed alikuwa akitumia muda mwingi kutoa mafunzo kwa wanamgambo na kuanda mipango ya kushambulia nchi za magharibi.

Alikuwa akitoa mafunzo kwa vijana wa Kisomali na Waislamu wengine waliokwenda Somalia kupata ujuzi na utaalamu wa kijeshi.

Profesa Nelly Lahoud, wa Kituo cha Kukabiliana na Ugaidi katika Chuo cha Kijeshi cha West Point nchini Marekani anasema, Fazul Mohammed alikuwa mtu muhimu katika kupanga operesheni za mtandao wa al-Qaeda.

Amesema kifo chake ni hasara kubwa kwa mtandao huo ingawa jukumu lake la kama mkufunzi bila shaka limelinufaisha kundi hilo.

Profesa Lahoud aliyepitia kitabu kilichoitwa 'Vita dhidi ya Uislamu: Hadithi ya Fazul Harun' ambacho huelezea maisha ya Fazul Mohammed, amesema mwanamgambo huyo ametoa mchango mkubwa kwa mtandao huo.

Kwa maoni yake, Fazul Mohamed alihisi kuwa aliwajibika kuwapa wenzake ujuzi aliokuwa nao.

Serikali ya Somalia imesema mamia ya wapiganaji wa kigeni walijiunga na mtandao huo, wakitokea nchi mbalimbali ikiwamo Afghanstan, Pakistan, nchi za Ghuba na Magharibi zikiwamo Marekani na Uingereza.

Baadhi yao wamekuwa viongozi wa makundi ya wanamgambo kama vile al Shabaab.

Maafisa wa usalama wa Magharibi pia walikuwa wakishuku kuwa Fazul Mohammed alikuwa akiratibu harakati zao pamoja na wanamgambo wa tawi la al Qaeda nchini Yemen.

Hilo ni tawi lililohusika na mashambulizi makali yaliyoendeshwa nalo katika nchi za magharibi, miaka ya hivi karibuni.

Waliomchunguza Fazul wanasema alikuwa mtu makinifu na mjanja na aliyezungumza kwa ufasaha lugha za Kiarabu, Kifaransa, Comoro, Kiswahili na Kiingereza.

Muaustralia Leah Farrellm mtaalamu wa masuala ya al-Qaeda, amesema kifo cha Fazul Mohamed kitaathiri uwezo wa al-Qaeda kuwepo katika kanda hiyo pamoja na operesheni zake katika nchi za kigeni.

Baadhi wa wataalamu wa masuala ya usalama, wanashuku kwamba mafunzo yaliyotolewa na Fazul Mohammed yamesaidia kupanga shambulio lililofanywa na kundi la al-Shabab mjini Kampala, Uganda mwaka 2010.

Shambulio hili lilisababisha vifo vya watu 79 waliokuwa wakiangalia kupitia runinga fainali ya Kombe la Dunia.

Hilo lilikuwa shambulio la kwanza kabisa kufanywa na al Shabab katika ardhi ya kigeni, kwa kile ilichosema kulipiza kisasi kwa Uganda kuchangia askari katika kikosi cha kulinda amani cha Umoja wa Afrika nchini Somalia (AMISOM).

Katika shambulio lingine, wanamgambo wa al-Shabaab walishambila kambi kuu ya jeshi la

Umoja wa Afrika (AU) Septemba 2009, mjini Mogadishu na kusababisha vifo vya askari 17.

Wakati meli ya MV Bukoba ilipozama katika Ziwa Victoria mwaka 1996, ikiwa imembeba mwanzilishi mwenza wa al-Qaeda, Abu Ubaidah al-Banshiri, Fazul alikuwa mmoja wa watu waliotumwa eneo la tukio, kujaribu kuthibitisha iwapo Abu Ubaidah ni miongoni mwa waliokufa, kitu ambacho hawakukosea

Mbali ya shambulio la balozi za Marekani mjini Dar es Salaam na Nairobi, mwaka 2002, Fazul alishutumiwa kuhusika na mashambulizi dhidi ya Hoteli ya Kikambala mjini Mombasa, Kenya na jaribio la kuidungua ndege ya Israel mjini humo.

Mapema mwaka 2007 wakati wa vita ya Somalia, Fazul alidhaniwa kuwa mpakani katika Kijiji cha Haya karibu na Ras Kamboni, sambamba na wanamgambo wa uliokuwa Umoja wa Mahakama za Kiislamu (ICU).

Januari 8, 2007, ndege ya Jeshi la Anga la Marekani, AC-130 ilishambulia eneo hilo, katika kile kilichoonekana kumlenga.

Maofisa wa Somalia walidai kifo chake kimethibitishwa kwa mujibu wa taarifa za Marekani kwa Serikali ya Somalia, lakini Balozi wa Marekani nchini Kenya, Michael Ranneberger, alikana kuuawa kwa Fazul katika shambulio hilo akisema kwamba msako dhidi yake na wenzake bado unaendelea

Mmoja wa wake zake na watoto wake walikamatwa wakijaribu kukimbilia Kenya kutokea Somalia.

Lakini Serikali ya Kenya ikawarudisha Somalia, ikikamata kompyuta ya mumewe iliyokuwa na taarifa nyeti.

Fazul anaaminika kuwa mtaalamu mkubwa wa kompyuta.

Kwa mara ya kwanza Fazul aliingia katika anga za wapelelezi wa Marekani baada ya mashambulizi dhidi ya balozi zake Kenya na Tanzania.

Ameelezwa na Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI) kama mtaalamu wa kutumia majina bandia aliyewakwepa kwa miaka mingi.

Anasemekana alielekea nyumbani katika visiwa vya Comoro vilivyopo Bahari ya Hindi mara baada ya shambulio hilo, lakini wakati makachero wa FBI walipombaini, alipanda ndege kuelekea nchi za Ghuba na kutoweka machoni mwao.

Fazul Abdullah aliyezaliwa visiwa humo katika miaka ya 1970, inaaminika alijiunga na al-Qaeda nchini Afghanistan katika miaka ya 1990.

Anasemekana alitumikia kipindi fulani akisoma nchini Saudi Arabia.

Kikosi cha Kupambana na Ugaidi cha Marekani kilipata hati ya kusafiria ya Fazul Abdullah Mohammed iliyotolewa mwaka 1990 mjini Moroni na kufufuliwa mwaka 1996 mjini Jeddah, Saudi Arabia.

Hati hiyo ilionesha alisafiri kwenda Mauritius mwaka 1990, Tanzania mwaka 1994 na Sudan mara kadhaa mwaka 1995 ambapo pia alikuwa Yemen na Kenya mwaka 1993 na mara kadhaa 1994 na 1995.

Inaonesha pia alikaa kwa mwaka mmoja nchini Pakistan 1991-1992.

Hakuwa akijulikana sana kabla ya hapo na tukio la mashambulizi ya mwaka 1998 nchini Tanzania na Kenya ndilo lililomuibua.

Alikuwa akishikilia uraia wa Comoro na Kenya ambako alioa na aliishi akifanya kazi kama mwalimu wa dini ya Kiislamu.

Article printed from Newhabari: **http://www.newhabari.com**

URL to article: **http://www.newhabari.com/2011/06/15/fazul-abdullah-mohammed-nguzo-muhimu-ya-al-qaida-iliyoanguka/**

Copyright © 2010 Newhabari. All rights reserved.

Liberté • Égalité • Fraternité
RÉPUBLIQUE FRANÇAISE

MINISTÈRE DES AFFAIRES ÉTRANGÈRES ET EUROPÉENNES

DIRECTION GENERALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des concours et examens professionnels
RH4B

CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCES A L'EMPLOI DE SECRETAIRE DES AFFAIRES ETRANGERES (CADRE D'ORIENT) AU TITRE DE L'ANNEE 2012

EPREUVES ECRITES D'ADMISSIBILITE

8 septembre – 14 septembre 2011

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures.
Coefficient : 2.
Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire.
Barème de notation des 3 épreuves : QCM 4 points, fiche 10 points, note 6 points.

– NOTE EN SWAHILI –

*Rédaction en **swahili** d'une note (350 mots avec une tolérance de plus ou moins 10%) à partir de documents ou d'informations en swahili. – **Durée (note et fiche de synthèse) : 2 heures 30 minutes.***

Ce dossier comporte 10 pages (page de garde non comprise).

*
* *

SUJET : Vous rédigerez une note en swahili sur la candidature de Christine Lagarde à la tête du FMI.

Imechapishwa na *RFI* (http://www.kiswahili.rfi.fr)

Christine Lagarde asikilizwa alhamisi Juni 23 na bodi ya uongozi wa IMF

Imefanywa tarehe *2011-06-23 13:25*
Na Ali Bilali
FRANCE-WASHINGTON
0

Waziri wa Uchumi wa Ufaransa Christine Lagarde, mgombea kwenye uadhifa wa ukurugenzi Ukuu wa Shirika la Fedha la Kimataifa(IMF), anatarajiwa kusikilizwa Alhamisi Juni 23, 2011 na bodi ya taasisi hiyo kubwa.

Mbali na ushindani kutoka Mexico na Agustín Carstens, pia mgombea huyo anakabiliwa na uchunguzi mpya katika mgogoro kati ya Club Lionnais na Bernard Tapie.

Christine Lagarde atasikilizwa Alhamisi Juni 23 na bodi ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) mjini Washington. Mgombea kwenye uadhifa huo uliachwa wazi na Dominique Strauss-Kahn aliejiuzulu baada ya kukabiliwa na tuhuma za ubakaji. Waziri huyo wa uchumi wa Ufaransa Christine Lagarde, atatakiwa kutowa maoni yake juu ya masuala yanayo likabili fuko hilo la fedha duniani na nchi wanachama wake. Atatakiwa pia kujibu maswala yote atayo ulizwa na bodi ya uongozi wa fuko hilo la IMF.

Christine Lagarde anashindana na Agustín Carstens ambae upande wake alisikilizwa Jumanne Juni 21 na Wanachama ishirini na nne. Wanachama hao watatakiwa kupata muafaka kati ya wagombea hao wawili. Ikiwa muafaka utakosekana watatakiwa kupigas kura na kumtangaza mshindi Juni 30

Christine Lagarde waziri wa uchumi wa Ufaransa anaewania uongozi wa IMF
Reuters

Source URL: http://www.kiswahili.rfi.fr/dunia/20110623-christine-lagarde-asikilizwa-alhamisi-juni-23-na-bodi-ya-uongozi-wa-imf

14.06.2011

Wawili wabakishwa kugombea ukuu wa IMF

Kinyanga'nyiro cha kuwania ukuu wa Shirika la Fedha la Kimaifa (IMF), sasa kimeingia hatua ya fainali kati ya Waziri wa Fedha wa Ufaransa, Christine Lagarde, na Gavana wa Benki Kuu ya Mexico, Augustin Carstens.

Bodi ya wakurugenzi IMF sasa imewabakisha wagombea hao wawili kuuwania wadhifa wa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, baada ya mgombea wa tatu kusshindwa kupenya kwenye mchujo. Gavana wa Benki Kuu ya Israel, Stanley Fischer, aliyekuwamo katika kinyang'anyiro hicho, ameangushwa na umri wake wa miaka 67.

Linapokuja suala la kugombea wadhifa huu kwa mara ya kwanza, umri ni sheria muhimu kufuatwa na IMF, ambapo kwa mujibu sheria hiyo Stanley hawezi kugombea kwa kuwa ameshavuuka miaka 65.

Sasa msimamo thabiti wa nchi za Ulaya kumuunga mkono Lagarde wa Ufaransa, unamuweka mwanasiasa huyo katika nafasi nzuri ya kuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la IMF kuziba pengo lililoachwa na Mfaransa mwenzake, Dominique Strauss-Kahn, aliyelazimika kujiuzulu mwezi uliopita kutokana, akikabiliwa na tuhuma za kujaribu kumbaka mtumishi wa hoteli, mjini New York.

Hata hivyo, Lagarde, mwenye umri wa miaka 55, amekiri kuwa nafasi hii anayoiomba ni jukumu kubwa sana."Hii ni changamoto kubwa sana, ninayodhamiria kuitekeleza kwa unyenyekevu wote na natumai mwafaka wa kiwango kikubwa utafikiwa."

Lagarde amezunguka dunia ili kujipigia debe na anaungwa mkono hasa na nchi za Ulaya ambapo yeye mwenyewe amekuwa anaishugulikia migogoro ya fedha kwa undani sana. Nafasi ya kuchaguliwa kwake ni kubwa kwani anaungwa mkono pia na Misri, Indonesia na nchi kadhaa za Afrika.

Mshindani wake, Agustine Carstens, ana dhamira ya kuuvunja mwiko wa miaka 65 iliyopita kwenye taasisi hii kubwa kabisa ya kifedha duniani, ambapo hakuna kiongozi wake mkuu aliyetoka mataifa yanayoendelea.

Alijipigia debe kwa waziri wa fedha wa Marekani, Timothy Geithner ambaye, hata hivyo, hakuhakikisha wala kukataa kumuunga mkono. Badala yake, Geithner amesema tu kwamba Carstens anachanganya kipawa juu ya mambo ya fedha na ustadi wa kisiasa.

Tokea IMF iundwe baada ya kumalizika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, nafasi ya ukurugenzi mkuu imekuwa ikishikiliwa na mtu kutoka barani Ulaya.

Ikiwa mtaalamu huyo wa uchumi aliyesomea Chuo Kikuu cha Chicago atafanikiwa kuchaguliwa, basi atakuwa mtu wa kwanza kutoka nje ya Ulaya kuuvunja mwiko huo wa IMF.

Hata hivyo, hata mwenyewe Carstens amekiri kwamba Lagarde ndiye mwenye nafasi kubwa ya kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu mpya wa IMF.

Bodi ya wakurugenzi ya taasisi hiyo imesema kwamba itakutana na wajumbe hao wawili kwa lengo la kukamilisha uchaguzi tarehe 30 ya mwezi huu.

Mwandishi: Abdu Mtullya/AFPE/RTRE/ZAR
Mhariri: Othman Miraji

| www.dw-world.de | © Deutsche Welle.

11 Juni, 2011 - Imetolewa 19:03 GMT

Gavana wa Israel kuwania cheo cha IMF

Gavana wa benki ya Israel, Stanley Fischer, alitangaza siku ya Jumamosi kwamba nia yake ni kuwania madaraka ya kuliongoza shirika la fedha ulimwenguni, IMF.

Kuna uwezekano mkubwa sasa ushindani utakuwa mkali mno kati yake na Christine Lagarde kutoka Ufaransa, na ambaye ilielekea alikuwa anaongoza katika kampeni ya kuitafuta kazi hiyo.

"Kuijitokeza nafasi nzuri, na pasipo kupanga, na ambayo huenda isijitokeze tena, katika kuwania nafasi ya kuiongoza IMF, na baada ya kufikiria kwa muda mrefu, nimeamua kuizingatia jambo hilo", Fischer alieleza katika taarifa yake.

"Haya ni licha ya utaratibu mgumu, na vikwazo ambavyo huenda vikajitokeza," alielezea.

Fischer, mwenye umri wa miaka 67, anatazamiwa huenda akawa ni mpinzani mkali wa waziri wa fedha wa Ufaransa, Christine Lagarde.

Katika kura ya maoni iliyoendeshwa na Reuters miongoni mwa wanauchumi, na iliyochapishwa mwezi Mei, kati ya wahusika 56, 32 walimuunga mkono Lagarde, na ambaye pia wengi katika muungano wa Ulaya wa EU wanadhani atafaa kuyasimamia madaraka hayo.

Stanley Fischer katika picha ya pili ya juu kuanzia kushoto

Fischer, wakati mmoja alikuwa ni naibu wa mkurugenzi mkuu wa IMF.

Anasifiwa na wengi kwa kuusaidia uchumi wa Israel kustawi, hasa kwa kupunguza viwango vya riba mapema mwaka 2008.

Tangu wakati huo, amelnua viwango hivyo mara kumi, katika jitihada za kuzuia kuporomoka kwa bei na mapato, na kuuwezesha uchumi kuendelea kustawi kwa asilimia 5 mwaka huu wa 2011.

BBC

Imechapishwa na *RFI* (http://www.kiswahili.rfi.fr)

Christine lagarde atangaza kugombea ukuu wa IMF

Imefanywa tarehe *2011-05-25 17:03*
Na Ali Bilali
Ufaransa-Umoja wa Ulaya
0

Waziri wa uchumi wa ufaransa Chritine Lagarde amejitangaza jumatano Mei 25 kuwa mgombea nafasi ya ukuu wa Shirika la Fedha Duniani, IMF kuchukua nafasi ya aliyekuwa mkuu wa shirika hilo Dominique Strauss-Kahn. Licha ya kuwa anaungwa mkono na idadi kubwa ya wajumbe katika Umoja wa Ulaya haimaanishi kuwa amekwisha shinda.

Ni rasmi sasa Chritine Lagarde atagombea uadhifa wa kuwa mkuu wa IMF. Tangazo hilo limetokea katika mkesha wa mkutano wa nchi 8 zilizoendelea duniani unaotarajiwa kufanyika Dauville. Upande wa Umoja wa Ulaya, kumemuwa na muafaka. Ujerumani, Uingereza, italia tayari vimemuunga mkono waziri huyo mfaransa.

Kamisheni wa wa umoja wa ulaya Jose Manuel Barosso aunga mkono kikamilifu mgombea huyo huku kamisheni wa Umoja wa Ulaya anaehusika na maswala ya Fedha na uchumi Olli Rehn amefhamisha kuwa " kufuatia hali ya sasa ya uchumi na madeni barani Ulaya, Mfaransa ana nafasi bora" Kulingana na duru kutoka Marekani, Marekani pia yatakiwa kuunga mkono mgombea huyo kutoka Umoja wa Ulaya.

Licha ya kwamba Christine Lagarde aonekana kuwa mgombea bora bado hajashinda kwani anadhoofishwa na kesi ya Bernard Tapi. Waziri huyo wa fedha anatuhumiwa makosa ya matumizi mabaya ya mamlaka. Kulingana na ripoti ya Mahakama ya Wakaguzi, ya mwaka 2007 alifanya maamuzi yaliokinyume na taratibu za kazi, ili kutatua mgogoro kati ya mfanyabiashara Bernard Tapie na Mota mikopo kuhusu mauzo ya kiwanda cha Adidas. Mzozo ambao ulimalizika baada ya serikali ya ufaransa kutowa kitita cha pesa za ulaya milioni 385.

kuhusiana na mkasa huo, Christine Lagarde alisema wakati wa mkutano na waandishi wa habari kwamba alikuwa na "imani" na "yuu mtulivu." Pia alisema kwamba "ataendelea kugombeakuwa mkurugenzi wa IMF hata kama utaanzishwa uchunguzi.Maamuzi juu ya kuendelezaq kesi hiyo utatolewa Juni 10 mwaka huu siku ambayo itakuw ay amwisho kupokea maombi ya wagombea wa IMF

Kufuati mfumo ambao usio rasmi uliokubaliwa tangu mwaka 1945 Uongozi wa benki ya Dunia unakwenda kwa Marekanihuku IMF ikiongowa na Ulaya. Lakini wakati huu, nchi zinazokuwa kiuchumi hazitaki kusikia mfumo huo. Wanataka kudhoofisha mfumo huo. Katika taarifa yake, wajumbe wa BRICs, China, India, Russia, Afrika Kusini na Brazil kuwa alisema: "Ni lazima kuachana na mfumo huo wa kizamani usio rasmi kuwa kiongozi wa IMF lazima

atoke Ulaya . "

Mexico imewasilisha jina la mkuu wa benki kuu Agustín Carstens, wakati mataifa ya Afrika Kusini na Kazakhstan, yanayoungwa mkono na Urusi, zaweza kuwasilisha majina ya wagombea wao. Waziri wa fedha wa Brazil Guido Mantega amesema kuwa uongozi wa IMF wapaswa kutolewa kukizingatiwa Ujuzi na utendaji kazi wa mgombea hapana kuzingatiwa Uraia wake. Katika kujibu, Christine Lagarde alisema kwamba kuwa raia wa Ulaya "kusichukuliwe kama kudhohofika"

Christine Lagarde akitangaza kuwania kuongoza IMF
REUTERS/Jacky Naegelen

Source URL: http://www.kiswahili.rfi.fr/dunia/20110525-mgombea-kwenye-uadhifa-wa-imf-chrstine-lagrde-ajitangaza

Imechapishwa na *RFI* (http://www.kiswahili.rfi.fr)

Christine Lagarde waziri wa fedha wa Ufaransa huenda akamrithi Dominique Strauss Kahn

Imefanywa tarehe *2011-05-20 16:50*
Na Ali Bilali
Ufaransa
0

Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Kimataifa la Fedha IMF latarajiwa kukutana ljumaa hii, Mei 20, 2011, mjini Washington kujadili mikakati ya kumrithi Dominique Strauss-Kahn. Tangu kukamatwa kwake Jumamosi Jumamosi iliopita mjini New York jina la Christine Lagarde, Waziri wa Uchumi wa Ufaransalimekuwa likitajwa kama mgombea bora anaefaa kutoka Umoja wa Ulaya.

Waziri wa fedha wa ufaransa Chritine Lagarde kwa zaidi ya miaka mitatu, ambaye anaongoza rekodi nchini Ufaransa, asifiwa na wenzake wote. Ufahamu wake wa masuala, uwezo wake wa kazi wakati wa mgogoro wa 2008, na kusikiliza katika vikao vya kimataifa, vinasababisha kutambulika. Utendaji wake wa kazi mika ya nyuma unafanya awe kwenye nafasi nzuri ya kuweza kuchaguliwa.

Kabla ya kuchukua majukumu katika serikali ya Ufaransa, Christine Lagarde alikuwa mwenyekiti wa ofisi ya mahakimu yenye sifa kubwa nchini Marekani. Christine Lagarde anaungwa mkono na mwenziwake wa Sweden, anawezakuwa pia kuwa ni mgombea anaependekezwa na Kansela wa Ujerumani Angela Merkel.

Tangu Mei 19, 2011 Gazeti la The New York Times limemueleza kama mgombea bora. Hata hivyo gazeti hilo limetaja na kukumbusha alivyo simamia kesi ya Bernard Tapie / Mkopo wa Credit Lyonnais. Idadi kubwa ya pesa kiasi ya Euro 385,000,000 ilitengwa kwa mahakama ya usuluhishi wa mfanyabiashara ambae alijihisi kuibiwa wakati wa mauzo ya Adidas kwa shirika la mkopo la Credit Lyonnais wakati inayomilikiwa benki.

Christine Lagarde anashutumiwa kuingilia kati na kutatua mgogoro ulioisababisha gharama kubwa kwa taifa. Mahakama yaweza kufanya utafitii katika miezi ijayo kuamua iwapo uamuzi huu ulikuwa halali.

Christine Lagarde atakuwa na kibarua kigumu kuongeza shirika lenye kuhitaji kiongozi mwenye fahamu zaidi na muadilifu katika uongozi wake.

Waziri wa Fedha wa Ufaransa Christine Lagarde
@Reuters

Source URL: http://www.kiswahili.rfi.fr/generali/20110520-christine-lagarde-waziri-wa-fedha-wa-ufaransa-huenda-akamrithi-dominique-strass-k-0

Imechapishwa na *RFI* (http://www.kiswahili.rfi.fr)

EU yapendekeza mwanachama wake kuwa mrithi wa Strauss-Kahn

Imefanywa tarehe *2011-05-19 15:25*
Na Zuhura Seif Mwera
UBELGIJI
0

Mjadala wa nani apewe jukumu la kuliongoza shirika la fedha duniani IMF umeibuka na tayari nchi za ulaya zimejitokeza na kupendekeza bosi mpya wa shirika hilo atoke miongoni mwa nchi wanachama wa Umoja wa Ulaya .

Muda mfupi baada ya Dominique Stauss Kahn kujiuzulu wadhfa wake mengi yamesikika juu ya nani atarithi wadhfa wake.

Msemaji wa rais wa tume ya umoja wa ulaya Pia Ahrenkilde-Hansen amesema msimamo wa bwana Jose Manuel Barroso kuhusu nani anastahili kuchukua nafasi hiyo uko wazi.

Bi. Ahrenkilde-Hansen amesema bwana Barroso anaamini kigezo muhimu si utaifa ila ni muhimu kwa mwanachama kutoka katika umoja huo kuchukua nafasi hiyo kwani umoja huo ndiyo unaotoa mchango mkubwa kwa IMF .

Bwana Barroso pia anaamini ni muhimu kuchagua mtu mwenye weledi ambaye ataungwa mkono kwa urahisi na wananchama wengi wa IMF.

China taifa la pili tajiri duniani inapendekeza wajumbe kutoka mataifa yanayokuja juu kiuchumi kupewa nafasi za juu za uongozi katika shirika la fedha duniani.Prof. Ibrahim Lipumba mwanasiasa na mchumi aliyebobea kutoka nchini Tanzania anaunga mkono hoja hii ya China.

Gavana wa benki kuu ya China Zhou Xiaochuan amesema uongozi wa IMF ni muhimu uzingatie mabadiliko ya uchumi katika nchi mbalimbali na lazma yawakilishe mataifa yanayokua kwa kasi kiuchumi.

Hayo yanajiri wakati ambapo timu ya mawakili wa aliyekuwa mkuu wa IMF DSK ikiendelea na harakati za kumkwamua kiongozi huyo katika tuhma za ubakaji.

Rais wa tume ya Umoja wa Ulaya Jose Manuel Barroso
EU

PROF. IBRAHIMU LIPUMBA [1]

Source URL: http://www.kiswahili.rfi.fr/ulaya/20110519-eu-yapendekeza-mwanachama-wake-kuwa-mithi-wa-strauss-kahn

Links:
[1] http://www.kiswahili.rfi.fr/prof-ibrahimu-lipumba